# UMUHIMU WA AGANO LA KALE

## Somo la 11



Neno *lako ni kweli* – Yohana 17:17

*Namba ya Whatsap: 0752965019/ +255 757 411 482*

# UMUHIMU WA AGANO LA KALE

Agano la Kale lina vitabu 39. Ingawa hiyo ni karibu robo tatu ya Biblia, wengi hawaioni kuwa muhimu. Kwa kweli wachapishaji wengi huchapisha Biblia zenye Agano Jipya tu. Isipokuwa kitabu cha Zaburi, kitabu cha Mithali, na labda kitabu cha Mhubiri, vitabu vingine kwa ujumla vinapuuzwa.

Wengi huchukulia Agano la Kale kama historia ya Israel na mapito yake, vita, watu binafsi, maneno yao, na maelezo mengi kuhusu mambo yaliyotokea zamani. Kwa nini haya yote yameandikwa? Je, Agano la Kale ni muhimu kwa Wakristo leo? Ndio, kwa sababu kadhaa.

**Sababu # 1**

"*Sheria ni **kivuli tu** cha mambo mema yajayo, wala **si** uhalisi wa mambo yenyewe*" (Waebrania 10:1) [1]. Mungu ana mpango kwa wanadamu, lakini kabla ya wakati wa Yesu, mpango huo haukueleweka. "Mambo mema yajayo" inarejelea kuwaokoa wanadamu kutoka katika tanzi ya dhambi na mauti. Imejikita katika kazi ya Yesu ya ukombozi kupitia kifo chake juu ya msalaba wa Calvary.

Mpango huu wa kimungu ungeeleweka baada ya kuja kwa mwana wa Mungu Yesu (Wagalatia 4:4). Ilionyeshwa tu katika namna ya kivuli kabla ya tukio hilo. "Vivuli" hivi ni kama vielelezo vidogo vilivyoundwa na wasanifu ili kuonyesha jinsi kitu kitakavyoonekana kikimalizika. Katika lugha ya Kibiblia hizi zinaitwa sura(mfano), kutoka katika neno la Kigiriki *tupos*. Agano la Kale limejaa mifano.

Hivyo mtume katika Waebrania sura ya 10 asema kwamba dhabihu zilizotolewa na Israel katika Siku ya Upatanisho ya kila mwaka zilikuwa tu mifano au vivuli vya kazi halisi ya upatanisho ili kukomesha dhambi ambayo ingetimizwa na Yesu. "*Haiwezekani damu ya mafahali na mbuzi kuondoa dhambi*" (Waebrania 10:4).

**Sababu # 2**

"*Kwa maana kila kitu kilichoandikwa* ***zamani,*** *kiliandikwa kutufundisha* ***sisi****, ili kwa saburi na faraja ya Maandiko tupate kuwa na tumaini*" (Warumi 15:4). Hii inatuambia mambo yaliyoandikwa katika Agano la Kale yalikuwa kwa ajili yetu sisi, Kanisa, kujifunza na kufarijiwa.

Ugonjwa unaweza kutibiwa. Kwa baridi, au homa, mtu hupata dawa inayofaa ya kutibu. Vivyo hivyo kuna magonjwa ya kiroho ambayo yanahitaji dawa za kiroho ili kuwezesha uponyaji wa kiroho. Tuseme imani ya mtu imekuwa dhaifu na imechoka. Dawa inayofaa ya kiroho ni "Ibrahimu." Soma imani yake kuu kwa Mungu, kiasi kwamba alikuwa tayari baada ya safari ndefu ya siku tatu ili kumtoa mwanawe mpendwa sana kama dhabihu kwa kutii maneno ya Mungu (Mwanzo 22:1-15). Hii inaongeza imani yetu kwa Mungu yule yule ambaye Ibrahimu alimwabudu.

Tuseme bidii ya mtu imeanza kupoa anapoishi katika ulimwengu akizungukwa na watu wasioamini? Dawa inayofaa ya kiroho ni "Danieli." Soma juu ya bidii yake kuu akiwa amezungukwa kwanza

na Wababiloni, kisha na Wamedi-Waajemi. Hakuogopa kamwe kusema juu ya Mungu wake kwa makafiri waliomzunguka. Hili linapaswa kutupa nguvu mpya ya kumtumikia kwa bidii Mungu yuleyule ambaye Danieli alimwabudu.

Tuseme matatizo mbalimbali ya maisha yanatufanya tukose subira, kunung'unika na kulalamika. Dawa inayofaa ya kiroho ni "Ayubu." Katikati ya mateso makali, alisema: "*Nilitoka tumboni mwa mama yangu nikiwa uchi, nami nitaondoka nikiwa uchi. BWANA alitoa na BWANA ametwaa; jina la BWANA lihimidiwe*" (Ayubu 1:21). "*Je! Tutakubali mema kwa Mungu, wala si udhia?*" (Ayubu 2:10). Shida na matatizo yetu si kitu ikilinganishwa na Ayubu. Maneno yake yanatupa nguvu ya kuistawisha subira tunapomtumikia Mungu yuleyule ambaye Ayubu alimwabudu.

Orodha ya dawa za kiroho ni pamoja na Nuhu, Musa, Yosefu, Daudi, Eliya, na wengine wengi, pamoja na mambo yaliyowapata na hadithi za maisha. Haya yote yanatutia moyo na kutufariji "sisi" (kanisa) **leo**!

**Sababu # 3**

"*Mambo hayo yaliwapata wao kwa **mifano**, yakaandikwa ili kutuonya sisi, tuliofikiliwa na utimilifu wa nyakati*" (1 Wakorintho 10:11). Mambo yaliyoandikwa katika Agano la Kale yanatoa "mifano" kwa ajili yetu "sisi," kanisa. Hili linaweza kueleweka vyema kwa kuzingatia mfano mmoja kutoka katika Agano la Kale.

Mwanzo sura ya 24 inaeleza mchakato ambao Ibrahimu alifuata ili kupata mke kwa ajili ya mwanawe mpendwa Isaka. Inaanza hivi: "*Wakati huu Ibrahimu alikuwa mzee na mwenye miaka mingi, na BWANA alikuwa amembariki katika kila njia. Akamwambia mtumishi wake mkuu wa vitu vyote katika nyumba yake, yule aliyekuwa msimamizi wa yote aliyokuwa nayo, 'Weka mkono wako chini ya paja langu'. Ninataka uape kwa BWANA, Mungu wa mbingu, na Mungu wa nchi, kwamba hutamtwalia mwanangu*

*mke katika binti za Wakanaani, ambao ninakaa kati yao, bali utakwenda katika nchi yangu na jamaa zangu na utamletea mwanangu Isaka mke."* Ili kwenda katika nchi ambayo watu wa ukoo wa Ibrahimu waliishi kungehitaji safari ndefu na ngumu.

*"Ndipo huyo mtumishi akachukua ngamia kumi miongoni mwa ngamia za bwana wake, akaenda, akichukua pamoja naye kila aina ya vitu vizuri kutoka kwa bwana wake. Akaondoka kwenda Aramu-Naharaimu, akashika njia yake mpaka mji wa Nahori"* (Mwanzo 24:10). Mtumishi huyo hakwenda mikono mitupu! Alikuwa na ngamia kumi waliobebeshwa "vitu vizuri." Alipofika Nahori, simulizi laendelea hivi: *"Akawapigisha magoti ngamia karibu na kisima cha maji kilicho nje ya mji; ilikuwa inaelekea jioni, wakati ambao wanawake wanatoka kwenda kuteka maji."* Safari yake iliishia kwenye kisima cha maji ikiwa inaelekea jioni wakati wanawake walipotoka kuteka maji kisimani. Huko akaketi na kusali: *"Ee BWANA, Mungu wa bwana wangu Ibrahimu … nimesimama karibu na chemchemi hii, na binti za watu wa mjini wanatoka kuteka maji. Basi na iwe hivi, nitakapomwambia binti mmojawapo, 'Tafadhali, utue mtungi wako nipate kunywa maji, kisha akasema, Unywe, nami nitawanywesha ngamia wako pia; basi na awe ndiye uliyemchagulia mtumishi wako Isaka."* (Mwanzo 24:12-14). Mtumishi huyo aliomba mwongozo kwa Mungu, na hata akapendekeza ishara ili apate uhakika kwamba alikuwa amemtambua kwa usahihi binti aliyechaguliwa. Ishara hiyo ililenga utayari wa binti kumsaidia.

Tunaendelea kusoma: *"Kabla hajamaliza kusali, Rebeka akatoka na mtungi wake begani. Alikuwa binti wa Bethueli mwana wa Milka, ambaye alikuwa mke wa Nahori, ndugu wa Ibrahimu. Binti huyo alikuwa mzuri sana wa sura, bikira; hakuna mwanamume aliyewahi kukutana naye kimwili. Aliteremka kisimani, akajaza mtungi wake, akapanda tena. Yule mtumishi akafanya haraka kumlaki, akasema, Tafadhali nipe maji kidogo katika mtungi wako. Kunywa, bwana wangu, alisema, na haraka akateremsha mtungi kwa mikono*

*yake na kumpa kinywaji. Baada ya kumpa yule mtumishi yale maji, binti akasema, 'Nitawatekea ngamia wako pia, hata watakapomaliza kunywa'. Kwa hiyo haraka akamimina mtungi wake kwenye birika, akakimbia kurudi kisimani kuteka maji zaidi, na kuteka maji ya kuwatosha ngamia wake wote."*

Mtumishi aliomba maji ya kunywa naye binti akakubali mara moja. Zaidi ya hayo, alijitolea kuteka maji kwa ajili ya ngamia kumi! Jinsi ilivyotimizwa kwa usahihi "Ishara" iliyoombwa na mtumishi wa Ibrahimu. Rebeka alifanya kazi kubwa sana ya kuteka labda mitungi kumi kwa ngamia wa kwanza, kisha kumi zaidi kwa wa pili, na kuendelea mpaka ngamia wa kumi akapokea mitungi yake kumi ya maji. "*Ikawa ngamia walipokwisha kunywa, yule mtumishi akatoa pete ya dhahabu yenye uzani wa beka (nusu shekeli) na bangili mbili za dhahabu uzani wake shekeli kumi*" (Mwanzo 24:22).

Baada ya mtumishi huyo kuona bidii ya Rebeka, mara moja alimpa zawadi ya vito vya dhahabu. Tunaweza kuwazia jinsi Rebeka alivyoshtuka na kushangaa! Kisha akamuuliza swali: *"Wewe ni binti wa nani? Tafadhali niambie, je, kuna nafasi katika nyumba ya baba yako ili tupate kulala? Akamjibu, Mimi ni binti Bethueli, mwana ambaye Milka alimzalia Nahori. Akaongeza, Tuna majani mengi na malisho, na mahali pa kulala usiku kucha*". Ikawa, Rebeka alikuwa mjukuu wa Nahori, ndugu wa Ibrahimu.

Baada ya kumkaribisha akae nyumbani kwake, alikimbia nyumbani ili kuwaambia watu wa familia yake habari hizi: "*Yule binti akapiga mbio na kuwaambia watu wa nyumbani mwa mama yake mambo hayo. Rebeka alikuwa na kaka aitwaye Labani, huyo akaharakisha ili kukutana na yule mtumishi kule kisimani. Mara tu alipoona pete na bangili kwenye mikono ya dada yake, na kusikia Rebeka akieleza vile mtu huyo alimwambia, alimwendea huyo mtumishi, akamkuta amesimama karibu na ngamia wake pale karibu na kisima. Akamwambia, karibu nyumbani wewe uliyebarikiwa*

*na BWANA, Kwa nini umesimama hapa nje? Nimeitayarisha nyumba na mahali pa ngamia.*" (Mwanzo 24:28-31)

Labani alifurahi kumwalika mtumishi huyo nyumbani kwao kwa kuwa si kila siku zawadi kuu na za gharama kubwa hutolewa na mgeni kisimani. Mara baada ya kukaa nyumbani, mtumishi huyo anajitambulisha kwa maneno haya: "*Mimi ni mtumishi wa Ibrahimu.*" Anaendelea kueleza kilichomleta katika safari hii ndefu.

"*BWANA amembariki bwana wangu kwa wingi, naye amekuwa tajiri. Amempa kondoo na ng'ombe, fedha na dhahabu, watumishi wa kiume na wa kike, ngamia na punda. Sara mke wa bwana wangu amemzalia mwana katika uzee wake, naye amempa kila kitu alicho nacho. Naye bwana wangu akaniapisha, akasema, 'Usimtwalie mwanangu mke katika binti za Wakanaani, ambao ninakaa katika nchi yao; bali uende kwa jamaa ya baba yangu, na ukoo wangu mwenyewe, ukamtwalie mwanangu mke huko. Ndipo nikamwuliza bwana wangu, Je! Ikiwa yule mwanamke hatarudi pamoja nami? Akajibu, BWANA, ambaye nimekwenda mbele zake, atamtuma malaika wake pamoja nawe, na kuifanikisha safari yako, ili upate kumtwalia mwanangu mke katika ukoo wangu na jamaa ya baba yangu. Kisha, utakapokwenda kwa jamaa yangu, utaachiliwa kutoka kwa kiapo changu hata kama watakataa kukupa wewe – utaachiliwa kutoka katika kiapo changu. Nilipofika penye chemchemi leo, nilisema, Ee BWANA, Mungu wa bwana wangu Ibrahimu, ukipenda, nakusihi unifanikishe safari hii niliyoiendea. Tazama, nimesimama karibu na chemchemi hii; binti akitoka kuteka maji, nami nikamwambia, Tafadhali nipe maji kidogo katika mtungi wako ninywe, naye akiniambia, Unywe, nami nitawatekea ngamia wako pia, basi na awe ndiye ambaye BWANA amemchagulia mwana wa bwana wangu. Kabla sijamaliza kuomba moyoni, Rebeka akatoka, na mtungi wake begani. Aliteremka kisimani, akajaza mtungi wake, akapanda tena., nami nikamwambia, Tafadhali nipe maji ninywe. Haraka akateremsha mtungi wake begani, akasema, Kunywa, nami nitawanywesha ngamia wako pia. Basi nikanywa, akawanywesha na ngamia pia. Nikamuuliza, wewe ni binti wa*

*nani? Akasema, Binti ya Bethueli, mwana wa Nahori, ambaye Milka alimzalia. Kisha nikatia pete usoni mwake na bangili mikononi mwake, nami nikainama na kumwabudu BWANA. Nikamtukuza BWANA, Mungu wa bwana wangu Ibrahimu, aliyeniongoza katika njia iliyonyoka, ili nimletee mwanawe mjukuu wa ndugu ya bwana wangu."* (Mwanzo 24:35-48)

Baada ya kuieleza familia hiyo habari yote kuhusu kwa nini alikuwa huko na jinsi alivyokuja kumchagua Rebeka, mtumishi huyo aliuliza swali kuu: *"Basi ikiwa mtamfanyia bwana wangu wema na uaminifu, niambieni; na ikiwa sivyo, niambie, ili nipate kujua nielekee njia ya kugeukia. Nao wakajibu bila kusita: "Hili limetoka kwa BWANA … huyu hapa Rebeka; umchukue, uende zako, na awe mke wa mwana wa bwana wako"* (Mwanzo 24:29-51).

Yule mtumishi akatoa zawadi zaidi kwa ajili ya Rebeka, kaka yake, na mama yake. "*Kisha yeye na wale watu waliokuwa pamoja naye wakala na kunywa na kulala huko. Walipoamka asubuhi yake, akasema, Nipeni ruhusa nirudi kwa bwana wangu. Lakini kaka yake na mama yake binti wakajibu, Na binti akae nasi siku kumi hivi; ndipo mwondoke. Lakini yule mtumishi akawaambia, Msinicheleweshe, kwa kuwa sasa Bwana amefanikisha safari yangu. Niruhusuni niende kwa bwana wangu."* (Mwanzo 24:54-56)

Asubuhi iliyofuata wakati wageni hawa wanataka kuanza safari yao ya kurudi Kanaani, familia inaomba safari hiyo kucheleweshwa kwa siku kumi. Lakini mtumishi huyo yuko imara katika azimio lake la kuondoka mara moja. "*Kisha wakasema, Hebu tumwite binti na tumwulize kuhusu hilo. Basi wakamwita Rebeka, wakamwuliza, Je! utakwenda na mtu huyu? Akasema 'Nitakwenda'."* (Mwanzo 24:57,58)

Hebu wazia imani ambayo Rebeka alionyesha! Yuko tayari kuhatarisha maisha yake ya baadaye kwa kwenda nchi ya mbali tena kwa mtu ambaye hajawahi kukutana naye hapo awali. Familia ilikubaliana na uamuzi wake nao wakamsidikiza njiani kwa baraka

hii: "*Ndugu yetu, na uongezeke uwe maelfu kwa maelfu; wazao wako wapate kumiliki malango ya adui zao. Ndipo Rebeka na vijakazi wake wakajitayarisha, wakapanda ngamia zao, wakaondoka pamoja na yule mtumishi*." (Mwanzo 24:60,61).

Rebeka akaondoka na yule mtumishi akawachukua vijakazi wake pamoja naye. Mwisho wa safari hiyo ndefu, walipofika Kanaani, nchi ya Ibrahimu, twasoma kwamba Isaka "*akatoka akaenda kondeni jioni moja ili kutafakari; naye alipotazama, akaona ngamia wanakuja; Rebeka naye akainua macho akamwona Isaka. Akashuka kutoka kwenye ngamia na kumwuliza mtumishi, Ni nani yule mtu aliyeko shambani anakuja kutulaki? Yeye ni bwana wangu, mtumishi akajibu. Kwa hiyo akachukua kitambaa chake na kujifunika. Kisha mtumishi akamwambia Isaka yote aliyoyafanya. Isaka akamleta katika hema ya Sara mama yake, akamwoa Rebeka. Basi akawa mkewe, naye akampenda; Isaka akafarijiwa baada ya kifo cha mama yake.* (Mwanzo 24:63-67)

Habari hii yote ya kihistoria ni "mfano." Ni kielelezo "kilichoigizwa" cha kitu maalum na muhimu kwa kanisa katika kipindi hiki cha Injili. Kama vile Ibrahimu alivyomtuma mtumishi wake kumtafutia mwana wake mpendwa Isaka bibi-arusi, kuna mchakato mwingine wa uteuzi wa bibi-arusi unaoendelea leo: "*Ninawaonea wivu, wivu wa Kimungu; kwa kuwa mimi naliwaposea mume mmoja, Kristo, ili niwalete kwake kama bikira safi*" (2 Wakorintho 11:2). Uteuzi wa "bibi-arusi" kwa ajili ya Yesu Kristo unarejelea kanisa: "*Na tufurahi na kushangilia na kumtukuza! Kwa maana arusi ya Mwana-Kondoo imekuja, na bibi-arusi wake amejiweka tayari*" (Ufunuo 19:7).

Hebu sasa tuchunguze kila mmoja wa watu katika simulizi hii ya kihistoria na kuona jinsi wanavyoonyesha au kufafanua jambo linalotukia leo.

**IBRAHIMU**

Ni wazi kwamba Ibrahimu, ambaye alikuwa tayari kumtoa mwanawe wa pekee Isaka, ni mfano wa Mungu Baba ambaye kwa hiari alimtoa "Mwana wake wa pekee" Yesu ili ulimwengu uokolewe (Yohana 3:16).

**ISAKA**

Isaka mwana wa Ibrahimu anawakilisha mwana wa Baba, yaani Yesu (Yohana 1:18).

**MTUMISHI MKUU**

Kama vile Ibrahimu alivyokuwa na mtumishi mkuu, Mungu pia anao. Kama vile mtumishi mkuu wa nyakati za kale hakujisemea mwenyewe, ndivyo ilivyo kwa "mtumishi mkuu" wa pekee wa Mungu: "*Yeye atakapokuja, huyo Roho wa kweli, atawaongoza awatie kwenye kweli yote. Hatanena kwa ajili yake mwenyewe; atanena tu yale atakayoyasikia, na mambo yajayo atawaambia."* ( Yohana 16:13 ) Mtumishi mkuu wa Ibrahimu alifananisha roho takatifu wa Mungu ambayo hutimiza makusudi yote ya Mungu. Kama vile Ibrahimu alivyomwagiza mtumishi wake asichague mke kati ya wale walioishi katika maeneo ya karibu, Mungu hakutaka bibi-arusi wa baadaye wa mwana wake atoke miongoni mwa malaika ambao anaishi nao. Mtumishi huyo alienda "nchi ya mbali," kama vile dunia ilivyokuwa mbali sana na mbinguni.

Mtumishi huyo alichukua ngamia pamoja naye na kusimama kwenye kisima cha maji. Maji katika Biblia ni ishara ya kweli. Yesu kwenye kisima alimwambia mwanamke Msamaria hivi: "*Kama ungalijua karama ya Mungu, na ni nani akuombaye maji, ungalimwomba, naye angalikupa maji yaliyo hai*" ( Yohana 4:10 ).

**REBEKA**

Huyu bikira mrembo anaenda kutafuta maji, kweli safi ya neno la

Mungu. Alionyesha nguvu nyingi na bidii katika utumishi wake usio wa kuchoka ili kuipata. Hakujitafutia kweli tu, bali pia aliitoa kwa hiari kwa wengine ingawa ilihitaji kujitolea kwake binafsi. Baada ya kufanya hivyo, alithawabishwa kwa zawadi za dhahabu, metali ambayo inafananisha mambo ya kimungu katika Biblia. Hata kabla ya kuwa mke wa Isaka, alipokea zawadi zenye thamani. Baada ya kukubali ombi la ndoa, zawadi zaidi zilitolewa kwake. Hizi zinafananisha zawadi nzuri na za ajabu tunazopokea kupitia roho mtakatifu tunapojitolea kuwa sehemu ya bibi-arusi wa Kristo.

Mtumishi pia alitoa zawadi za **vito vya fedha**. Fedha inawakilisha kweli ya Mungu ya thamani: *"Maneno ya BWANA ni safi (hayana kasoro), kama **fedha** iliyosafishwa katika tanuru ya udongo...."* (Zaburi 12:6). Naye akatoa zawadi za **vito vya dhahabu**. Dhahabu inawakilisha ahadi za kimungu, hasa za kufanywa "washiriki wa asili ya uungu" (2 Petro 1:4). Mwaliko huu wa "dhahabu" kwa wokovu mkuu wa mbinguni sasa unatolewa kwa kundi la "kanisa".

Mtumishi pia alitoa **zawadi za mavazi**. Hii inaashiria "Joho la haki " ambalo hufunika dhambi na sasa linalotupa kuifikilia "kiti cha enzi cha neema ya mbinguni" na kumfanya mtu "kuhesabiwa haki": [BWANA] "amenivika mavazi ya wokovu, na kunipamba kwa joho (vazi) la haki....." (Isaya 61:10). Joho hili linawakilisha neema ya Mungu ya kuhesabiwa haki na kufunika dhambi kwa damu ya dhabihu ya ukombozi ya Yesu msalabani. Hivyo Kanisa linapokea karama hizi zote za kiroho kwa huduma ya Roho Mtakatifu kama ilivyooneshwa na mtumishi wa Ibrahimu.

Rebeka alipoulizwa ikiwa angeenda, bila kusita alisema ataenda. Hii inaonyesha imani na uaminifu wa kundi la Kanisa ambao wako tayari kuwa bibi-arusi wa Bwana Yesu na kufuata nyayo zake popote pale ambapo wanaweza kuongozwa. Hivi ndivyo Petro afafanuavyo

mtazamo wao: "*Ingawa hamjamwona, mnampenda; na ijapokuwa hamwoni sasa, mnamwamini na kujawa na furaha isiyoneneka yenye utukufu usioelezeka*" (1 Petro 1:8).

Hata baraka ambayo Rebeka alipokea kutoka kwa familia yake ni ya maana: "*Na uongezeke uwe maelfu kwa maelfu*." Hakuna mwanamke anayeweza kuzaa "maelfu kwa maelfu." Lakini kanisa, mfano wa Rebeka, litakuwa Eva wa pili kwa mumewe, "Adamu wa pili" (1 Wakorintho 15:45). Yesu na kanisa pamoja watatoa uzima na baraka kwa ulimwengu katika ufufuo. Ulimwengu wa wanadamu utakuwa hawa "maelfu kwa maelfu" ya watoto!


Safari ya Rebeka chini ya ulinzi wa mtumishi mkuu wa Ibrahimu inawakilisha "safari ya ya hapa duniani" ya kanisa katika kipindi hiki cha Injili. Anaiacha nchi yake na kusonga mbele kuelekea kanaani ya mbinguni. Mwishoni mwa safari, Rebeka anaolewa na Isaka, kilele cha hadithi kuu ya upendo. Vivyo hivyo hadithi ya upendo ya Yesu na kanisa inaishia kwenye arusi kuu ya Mwana-Kondoo (Ufunuo 19:7).

Hivyo tumechunguza "mfano," picha(kivuli), inayopatikana katika Agano la Kale ambayo inatufundisha kweli kuu za kimungu! Kuna mifano mingi zaidi katika Agano la Kale kama vile:

- Israel na utumwa wao na ukombozi kutoka Misri kupitia Musa.
- Safari yao ya kutoka Misri kwenda Kanaani.
- Wimbo Ulio Bora wa Sulemani unaoonyesha uhusiano wa Bwana na kanisa lake.
- Hema ya kukutania na dhabihu zake (Waebrania 9:9,10).
- Sheria, Pasaka, Yubile, na mengine mengi.

Vito hivyo vya kweli y a kiroho vimehifadhiwa katika Agano la Kale na tutajifunza mengi yao katika masomo yajayo.

**-Amina-**



*Kwa Masomo zaidi Tuandikie Ujumbe kupitia:*

*Email: thekingdom1_6@gmail.com au isayaruhala25@gmail.com*

*©HAKIUZWI*

***Namba ya Whatsap: 0752965019/ +255 757 411 482***